JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# MRADI WA UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI TANZANIA (P159192)

## Kutangazwa Kwa Utaratibu wa Uhamishaji Makazi na Shughuli za Kijamii (RPF)

**Desemba, 2020**



## 1. UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania (GoT) inatekeleza Miradi Ushirikiano wa Umma na Binafsi (PPPs) ili kujenga miundombinu na kuimarisha huduma za umma. Utekelezaji unaongozwa na Sera ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) iliyoidhinishwa mwaka 2009, Sheria ya PPP Sura ya 103 na Kanuni za PPP za 2020.

Mradi unaopendekezwa wa wa Mradi wa Ushirikiano wa Umma na Sekta Binafsi (TPPP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ni dola milioni 14 na utasaidia Wizara, Idara na Wakala wa Serikali (MDAs) na mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kutekeleza Programu ya PPP. TPPP itasaidia Kituo cha PPP kilichopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), Kitengo cha PPP (*PPP Node)* kilichopo Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mamlaka za Serikali (CA) zinazotekeleza miradi. TPPP itazingatia yafuatayo:

a) Uandaaji na ununuzi wa miradi ya PPP,
b) Kuimarisha misingi ya PPPs (kujenga uwezo), na
c) Ufuatiliaji na Tathmini.

Miradi ya PPP inayostahiki msaada wa TPPP itajumuisha (i) miradi mikubwa, kama vile ya miundombinu ya usafirishaji, uzalishaji wa umeme, usambazaji wa maji, afya, elimu, na habari, mawasiliano na teknolojia, na (ii) miradi midogo midogo, kama vile masoko ya kisasa , vituo vya basi na daladala, usimamizi wa takangumu na maji, na hosteli za wanafunzi. Miradi mingine itaboreshwa na mininge itakuwa mipya kabisa. Kazi za TPPP zitangingatia mahitaji lakini hazitakwenda Zaidi ya wigo wa madhara ya kama itakavyoinishwa.

## 2. MALENGO

Malengo ya Utaratibu wa Uhamishaji wa Makazi na Shughuli za Kibinadamu (RPF) ni:

i. Kuanzisha utaratibu wa kuhamisha makazi na fidia pamoja na taratibu za utekelezaji;
ii. Kufafanua mfumo wa kisheria na wa kitaasisi unaohusu kuhamisha makazi, fidia na uboreshaji;
iii. Kulinganisha sheria za Tanzania na Sera ya Uendeshaji inayohusu Uhamishaji wa Makazi ya Benki ya Dunia (OP 4.12) na kubainisha mapungufu;
iv. Kufafanua vigezo vya kubainisha wanaostahili kutambuliwa kama waathirika wa mradi (PAPs) na stahiki zao, kwa kuzingatia sheria ya Tanzania na Sera ya Uendeshaji ya Benki ya Dunia (OP 4.12);
v. Kuelezea mchakato kwa ajili ya kuandaa, kutekeleza, kufuatilia na kufanya tathmini kwa ajili ya kuwa na Mipango Kazi ya Kuhamisha Makazi;
vi. Kuelezea hatua za mashauriano na njia shirikishi zinazowahusisha waathirika miradi (PAPs) na wadau wengine munhimu; na
vii. Kuweka taratibu za kufuatwa kwa ajili ya kufikisha malalamiko na namna ya kutatua migogoro.

Sambamba na Sera hii ya Kuhamisha Makazi, pia Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) umeandaliwa kwa ajili ya TPPP. ESMF imetengeneza utaratibu wa namna ya kufuatilia masuala ya Mazingira na Jamiii na namna ya kuandaa Tathmini za Athari za Mazingira nad Jamii (TAM) na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMP).

## 3. MCHAKATO WA UTEKELEZAJI WA RPF

i. Miradi yote ya PPP itatathiminiwa kwa kina kwa ajili ya kuhakikisha kuwa athari zinazoweza kujitokeza kutokana na uhamishaji wa makazi usio wa hiari kama vile kuwahamisha watu kwenye majengo au vikwazo vya kuwafanya wasipate huduma na kipato kwa ajili ya ustawi wao. Tathmini ya awali itafanyika kwa kutumia fomu maalumu ya ukaguzi wa masuala ya mazingira na jamii iliyomo kwenye ESMF. Kulingana na majibu ya tathimini hiyo, mamlaka inayohusika na umiliki wa miradi ya PPP itaandaa RAP au ARAP itakayotumika kusimamia zoezi la kuhamisha watu kwenye makazi yao na kuwalipa fidia watakaoathirika na mradi kabla ya kuanza kwa mradi huo. ARAP ni chapisho fupi la RAP au ni muhtasari wa RAP ambao unaandaliwa kwa miradi ya PPP ambayo itakuwa imeathiri watu wachache wanaotakiwa kuhamishwa, au kwa watu walio chini ya 200 watakaotakiwa uhamishwa.[1]

ii. Miradi ya PPP itakayosaidiwa  na TPPP itakuwa kwenye ardhi inayomilikiwa na mamlaka iliyoingia mkataba wa usimamizi wa mradi. Tathimini ya TPPP itahusu masuala ya kisheria ya upatikanaji wa ardhi kwani Mamlaka inayosimamia mkataba wa PPP inatakiwa kuonyesha nyaraka zote zinazohusu mchakato wa upatikanaji wa ardhi hiyo. Miradi ya PPP itafanyika kwenye maeneo ya miji mikubwa na maeneo ya pembezoni mwa miji na haitaendelezwa kwenye maeneo ambayo jamii zitapoteza maeneo yao.

iii. Baadhi ya miradi ya PPPs inayosimamiwa na TPPP itahusisha uhamaji usio wa hiyari na/au vikwazo vinavyohusu upatikanaji wa huduma na kipato kwa muda. Miradi mingine itahusisha athari kubwa za kiuchumi kwa kuhamisha watu kwa muda kutoka kwenye maeneo au majengo yao ya sasa na kwenda sehemu nyingine wakisubiri ujenzi ukamilike (mfano wa hili ni kama vile kuwahamisha wafanyabiashara wadogo wadogo kutoka kwenye soko la zamani na kupelekwa kwenye jengo la muda na baadaye kurejeshwa kwenye soko jipya lililojengwa kwa PPP). Na wakati mwingine, mradi wa PPP unaweza kuwaathiri watu waliopanga au kukodisha ardhi inayomilikiwa na mamlaka inayosimamia mradi au watu waliovamia na kujenga vibanda kwenye eneo linalomilikiwa na mamlaka inayotekeleza Mradi.

---

[1] Sera ya Usalama wa Miradi ya Benki ya Dunia OP 4.12 – kuhusu kuhama makazi kwa lazima inaeleza kuwa, “endapo hakutakuwa na madhara makubwa ya mradi kwa watu wengi, au watakaohamishwa ni chini ya watu 200 , basi Mpango Mdogo wa Kuhamisha Makazi unaweza kukubalika kutumika…Madhara yanayotambulika kuwa ni madogo endapo wale watakaoathirika na mradi hawajahamishwa ni wanapoteza chini ya asilimia 10 ya mali zao”.

iv. Kwa miradi ya PPP itakayohusisha kuwahamisha wafanyabiashara wadogo wadogo, shughuli za kibiashara au kiuchumi, basi tathimini ya RAP/ARAP itaonesha hatua za kufuatwa wakati wa kuwahamisha kwa muda kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Hatua nyingi zilizopendekezwa kwenye RAP/ARAP zitachukuliwa mapema kabla ya kuanza ujenzi. Shughuli zinazoweza kufanyika kabla ya kuanza ujenzi ni pamoja na kuhakikisha kuwa eneo la ujenzi linafikika vizuri kwa kuhamisha makazi holela ya wavamizi wa eneo linalomilikiwa na Mamlaka ya Utekelezaji wa Mradi na kuwahamisha wafanyabiashara wadogo wadogo kwenda kwenye eneo la muda lililotengwa kwa ajili yao. Hatua nyingine zinazoweza kupendekezwa kwenye RAP/ARAP ambazo ni pamoja na kuwarejesha wafanyabiashara kwenye jengo jipya zitatekelezwa tu baada ya ujenzi wa jengo kukamilika;

v. Mamlaka ya Utekelezaji wa Mradi itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa Sera ya Uhamishaji wa Makazi inatekelezwa kwa kila mradi wa PPP, ikiwemo kuandaa na kuidhinisha RAP/ARAP kabla ya kuanza mchakato wa zabuni ya kumtafuta mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya kushiriki kwenye mradi wa PPP. RAP/ARAP na hatua zake zilizopendekezwa zitafanyiwa mapitio na Kitengo cha PPP pamoja na Benki ya Dunia kabla ya kuhitimishwa kwa ajili ya kuhakikisha zinaendana na RPF, na zitaidhinishwa tu endapo zinaendana na matakwa ya Sheria na matakwa ya Benki ya Dunia.

vi. RAP/ARAP zitaandaliwa kabla ya kuanza mchakato wa zabuni ya kumtafuta mbia wa mradi wa PPP kutoka sekta binafsi. Kimsingi tathmini hizi zinaandaliwa wakati mmoja na upembuzi yakinifu na tathmini za Mazingira na Jamii za miradi ya PPP. Hadidu za Rejea (ToR) kwa ajili ya RAP/ARAP zitaandaliwa kufuatia uchunguzi wa Mazingira na Jamii kuhusiana na mradi wa PPP. Hadidu za Rejea za RAP zitazingatia mwongozo wa Hadidu za Rejea kwa ajili ya RAP zilizomo kwenye Sera hii ya Kuhamisha Makazi. Mwongozo wa Hadidu za Rejea za RAP/ARAP utatafsiriwa kuangalia athari za kila mradi wa PPP. Upembuzi yakinifu mara nyingi utatanguliwa na upembuzi wa awali unaojumuisha uchunguzi wa kujiridhisha kuhusu masuala ya Mazingira na Jamii, ambayo yatatoa picha ya namna ya kuandaa Hadidu za Rejea za RAP/ARAP.

vii. Kabla ya kumpata mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya mradi wa PPP kwa kusaidiwa na TPPP, Mamlaka ya Utekelezaji wa miradi itatakiwa kuwasilisha Kitengo cha PPP na Benki ya Dunia bajeti halisi iliyoandaliwa kwa ajili ya kugharamia uhamishaji wa muda wa makazi au kuboresha hali za maisha ya watu. Msaada wa TPPP kwa ajili ya zabuni na kumpata mbia kutoka sekta binafsi utatolewa tu baada ya kuona mchanganuo wa gharama za kuhamisha makazi kwenye hiyo bajeti.

viii. Miradi yote ya PPP inayosimamiwa na TPPP itatakiwa kuandaa Hadidu za Rejea kwa ajili ya Tathmini za Athari za Kimazingira (ESIA). Mamlaka inayohusika na mradi itaandaa Hadidu za Rejea kwa ajili ya ESIA pamoja na Hadidu za Rejea kwa ajili ya RAP/ARAP kwa mujibu wa matakwa ya Sera ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF), kuhakikisha wadau wanashirikishwa wakati wa usimamizi wa mazingira na jamii katika mradi wa PPP. Maandalizi na utekelezaji wa ESIA utazingatia matakwa ya ESMF.

ix. Washauri wa miradi ya PPP na wataalamu wengine waelekezi wanaotoa ushauri kwa miradi ya TPPP baada ya kukidhi matakwa yaliyoorodheshwa. Mathalani hawatakuwa na msaada kwa miradi yenye vihatarishi vya daraja A kutokana na mwongozo wa Benki ya Dunia kama miradi chini ya TPPP. Ndio maana miradi inayopendekezwa ya PPP itafanyiwa tathimini ya awali (Screening) kwa vigezo vya athari za mazingira na jamii kama inavyoelekezwa kwenye ESMF.

## 4. TARATIBU ZA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

i. Sera ya Kuhamisha Makazi (RPF) imeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia malalamiko (GRM). Kuna nyenzo muhimu za kuwawezesha wadau kuwasilisha malalamiko waliyo nayo kuhusiana na utaratibu wa kuhamishwa na fidia, na ikionekana kuna ulazima, basi hatua za kurekebisha hali hiyo zitachukuliwa mara moja. GRM inatoa maelekezo kuhusiana na hatua za kufuatwa kwa ajili ya kushughulikia malalamiko yote yanayohusu usimamizi wa masuala ya Mazingira na Jamii ya miradi ya PPP, ikiwemo kushughulikia malalamiko yanayohusu uhamaji usio wa hiyari. Utaratibu huu ni muhimu kwa ajili ya kuweka uwazi katika michakato ya uhamishaji wa watu na kazi yao. GRM inazo pia taratibu za kushughulikia ukatili wa kijinsia (GBV) ukiwemo utaratibu wa kutoa taarifa kwa siri kwa kulinda usalama na maadili wakati wa kuandikisha kesi zinazohusu ukatili wa kijinsia.

ii. Utaratibu wa kushughulikia malalamiko (GRM) katika mradi wa PPP utatokana na taratibu na michakato ya kisheria ya kushughulikia malalamiko. Huu si utaratibu mpya unaolenga kuchukua nafasi ya taratibu za kisheria ambazo tayari zipo, bali unatoa nafasi ya uwazi na maridhiano ya pamoja na ukilenga zaidi kutatua kwa haraka malalamiko yanayopokelewa pasipo kutumia muda mwingi na gharama kubwa kupitia njia za kisheria na kimahakama.

iii. Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko uliopo kwenye Sera ya Kuhamisha Makazi (RPF) ni mchakato wa msingi unaosaidia pia kuandaa TAM na RAP/ARAP. Utaratibu huu unatoa nafasi ya kuimarisha uhusiano mzuri kwenye jamii unaosaidia watu kutekeleza sheria zinazohusu haki za wale wanaopoteza mali zao ndani ya Tanzania na matakwa ya Sera ya Uendeshaji wa Miradi ya Benki ya Dunia 4.12 kuhusiana na uhamaji usio wa hiyari.

## 5. KUJENGA UWEZO

i. Sera ya Kuhamisha Makazi imeandaliwa kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusiana na masuala ya Mazingira na Jamii. Tathmni ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA) itafanywa na Mamlaka zinazohusika na Miradi kwa kugharimiwa na TPPP. Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA) itafanyika kabla ya kuanza kwa TAM na RAP/ARAP.

ii. Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo kuhusiana na masuala ya Mazingira na Jamii itakuwa sehemu ya mpango mpana wa kujengea uwezo utakaoandaliwa kwa ajili ya Mamlaka zinazohusika na miradi inayosimamiwa na TPPP.

## 6. UTOAJI WA TAARIFA KWA UMMA NA USHIRIKISHWAJI WA WADAU

i. ESMF na RPF pamoja na nyenzo nyingine za usalama wa miradi kama vile ripoti za Tathmini za Athari za Mazingira na Jamii, ESMP, RAP na ARAP za kila mradi zitapitishwa na Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia na kutolewa kwa umma; na zitakuwa zikipatikana kupitia tovuti (mfano tovuti ya mradi husika wa PPP na ofisi mbalimbali na tovuti za Mamlaka zinazosimamia miradi) na kutakuwa na tafsiri ya muhtasari wake katika lugha inayozungumzwa kwenye eneo husika kwa kuzingatia utamaduni wa wenyeji. Zitawekwa pia kwenye tovuti za vitengo husika vya PPP na ile ya Benki ya Dunia. Endapo kutakuwa na mabadiliko yoyote katika nyaraka hizi basi utaratibu ule ule wa kuzipitisha utafuatwa. Wadau walishirikishwa ili kupata maoni yao na hoja zao kuhusiana na ESMF na RPF. Hili lilifanyika kwa awamu mbili. Wadau waliombwa ushauri wao juu ya miradi ya mfano ya PPP inayokuwa inapangwa kuwa chini ya usimamizi wa TPPP wakati wa kuanda pembuzi yakinifu za awali za miradi 22 ya PPP iliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Awamu kadhaa za mashauriano zilifanyika mfululizo kwa ajili ya kujadili na kushughulikia masuala muhimu yaliyoibuliwa kati ya Juni 2017 na Julai 2018. Ziara za kutembelea maeneo ya miradi zilifanyika kwa lengo la kuangalia hali za Mazingira na Jamii kwenye Mamlaka za Utekelezaji wa Miradi, taratibu za kitaasisi, uwezo wa kusimamia masuala ya Mazingira na Jamii, na masuala mahususi ya Mazingira na Jamii yanayohusu PPP.

ii. Vikao vya mashauriano vilijadili pia kuhusu uhitaji wa kuwa na PPP, muundo wake wa uendeshaji, utayari wa kulipa, muundo wa ujenzi, masuala mahususi ya eneo husika, uhamishaji wa muda wa makazi, na changamoto zinazokabili majengo ya sasa ya kutolea huduma. Maoni ya wadau yalitumika wakati wa kufanya mapitio ya ESMF na RPF yaliyofanyika Dodoma kati ya tarehe 5 – 9 Novemba, 2018 na tarehe 20 – 21 Februari, 2019. Wadau walihimizwa kutoa maoni yao kwenye majadiliano ya wazi na wenzao, na warsha hizo ziliendeshwa na maofisa kutoka TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango wanaohusika na usalama wa miradi, na waliomba kupokea maoni kutoka kwa mameneja wa usalama wa miradi wa Mamlaka za Utekelezaji wa Miradi (mfano Mamlaka za Serikali za Mitaa). Ushirikishwaji wa wadau utaendelea kufanyika kipindi chote cha mradi wa PPP unaosimamiwa na TPPP.

*Mchoro 1.1 Mzunguko wa Mradi wa PPP*



**KUTANGAZWA KWA RPF**

RPF sasa inatolewa kwa umma na itapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), TAMISEMI (kitengo cha PPP) na Kituo cha Habari cha Benki ya Dunia (Info-shop).

Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kupitia anuani ifuatayo:


Katibu Mkuu
Wizara ya Fedha na Mipango,
Mji wa Serikali – Mtumba;
Mtaa wa Hazina,
S. L. P 2802
40468 **DODOMA**
Dodoma
Barua Pepe: ps@mof.go.tz